الأخلاق في الإسلام - سواحيلي

# TABIA KWENYE UISLAMU




جمعية الدعوة بالزلفي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

295



هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ ـ فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

# TABIA KWENYE UISLAMU

## الأخلاق في الإسلام - سواحيلي

Kimetasiriwa na Kuhakikiwa na:
Abubakar Kassimu Abubakar
Ally Nassoro Ally
Abdallah Ally Chumbe
Yassir Salim

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
هاتف: 966 164234466 ـ فاكس: 966 164234477

# الأخلاق في الإسلام - سواحيلي
**أعده وترجمه للغة السواحيلية**
**جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي**
**الطبعة الأولى: ١٤٤٤/٠٦ هـ**


**ⓒ جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي ، ١٤٤٤هـ**

***فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر***

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
الأخلاق في الإسلام / لغة السواحلية. / جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي .- الزلفي ، ١٤٤٤هـ
٣٦ ص ؛ ..سم

ردمك: ٩-١٤-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨

١- الاخلاق الاسلامية ٢- الاداب الاسلامية أ.العنوان
ديوي ٢١٢,١ ١٤٤٤/٥٨٢٧

**رقم الإيداع: ١٤٤٤/٥٨٢٧**
**ردمك: ٩-١٤-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨**

بسم الله الرحمن الرحيم

# Utangulizi

Sifa Njema zote ni Zake Allah, na Rehema na Amani ziwe juu yake Mjumbe wa Allah. Ama baada ya hayo:

Tunamshukuru Allah Mtukufu kwa kutuneemesha neema ya Uislamu, na Akatuhimiza sana kushikamana na tabia njema na Akaweka malipo makubwa juu yake.

Tabia njema ni sifa miongoni mwa sifa za Manabii na waja Wema, kwa kuwa zinapelekea kupandishwa mtu daraja. Hakika Allah Mtukufu Amemsifu Mtume wake Muhammad kupitia ayah ambayo imekusanya tabia njema zote. Allah Mtukufu Amesema: *"**Na hakika wewe upo juu kwa tabia njema**.*" [al - Qalam: 4].

Tabia njema huleta upendo na mshikamano. Tabia mbaya huzalisha kuchukiana na kuhusudiana. Athari za mwenye tabia nzuri zipo wazi katika Dunia na Akhera. Allah Amemkusanyia mtu huyo kati ya *Taqwa* (Uchamungu) na Tabia nzuri. Mtume,

Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *"Mengi ambayo yatawaingiza watu peponi ni kumcha Allah na kuwa na Tabia njema." [Ameipokea Tirmidhi na Haakim]*.

Tabia njema: Ni kuwa na uso wa bashasha, kutenda mazuri na kutowaudhi watu. Haya Pamoja na maneno mazuri anayojilazimisha Muislamu, kuidhibiti na kuificha hasira yake, na kuvumilia maudhi. Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *"Nimetumwa kwa ajili ya kukamilisha Tabia njema."* [Ameipokea Ahmad, al-Bayhaqy na al-Haakim na ameisahihisha].

Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - alimuusia Abu Hurairah Allah Amridhie, *"Ewe Abu Hurayrah! Jilazimu na tabia njema."* Abu Hurayrah akasema, "Tabia njema ni zipi ewe mjumbe wa Allah?" Akasema: *"Ni kumuunga ndugu yako aliye-kukata, kumsamehe aliyekudhulumu na kumpa aliyekunyima."* [Ameipokea al-Bayhaqy katika Kitabu chake *Shuab*].

Angalia ndugu yangu Muislamu hii athari kubwa na thawabu nyingi za hii sifa tukufu. Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema,

*“Hakika Mtu hufikia daraja la mfungaji mwenye kusimama usiku kutokana na Tabia yake njema.”* [Ameipokea Ahmad]. Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, ameifanya Tabia njema kuwa ni miongoni mwa ukamilifu wa Imani ya mtu, akasema: *“Mkamilifu wa Imani kwa waumini ni yule mzuri wao kitabia”*.

Zingatia ndugu yangu kauli ya Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, *“Mtu anayependeza zaidi kwa Allah ni yule ambaye anawanufaisha watu. Na matendo yanayopendeza Zaidi kwa Allah Mtukufu ni furaha ambayo utaingiza kwa ndugu yako Muislamu, au ukamtatulia tatizo, au ukamlipia deni, au ukamuondolea njaa. Na kwenda kumsaidia ndugu yangu Muislamu katika shida, inapendeza zaidi kwangu kulikoni kujilazimisha kukaa msikitini kufanya ibada muda wa mwezi mzima.”* [Ameipokea Twabarany].

Ndugu yangu Muislamu, neno laini jema ulisemalo unapata malipo mema, na inakuwa ni sadaka yako. Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *“Na neno jema ni sadaka.”* [Wameafikiana Bukhary na Muslim kuwa ni Sahihi]. Na yote hayo ni kwa sababu neno jema lina athari nzuri. Kwani mioyo

huwa karibu, nafsi hupendana na huondoa kutengana.

Maelekezo ya kiutume katika kuhimiza Tabia njema na kuvumilia maudhi ni mengi, miongoni mwa hayo ni: Kauli yake Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, *"Muogope Allah popote uwapo, na fatilia ovu ulilolitenda kwa kutenda jema italifuta ovu hilo, na uamiliane na watu kwa tabia njema."* [Ameipokea al-Tirmidhy].

Tabia njema ni lazima kwa Muislamu kila sehemu na wakati wowote, hilo humpendezesha kwa watu, humuweka karibu nao kwa kila njia anayoipita, na kila sehemu anayo kwenda. Hata tonge analolinyanyua kumlisha mkewe hulipwa kwa kufanya hivyo katika Uislamu. Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *"Na hakika chochote unachokitoa katika matumizi ni sadaka, mpaka tonge ulilolinyanyua kwenye kinywa cha mke wako (ni sadaka)*." [Ameipokea Bukhary].

Ndugu yangu kipenzi! Waumini ni Ndugu, inapasa kwa Muislamu kumpendelea ndugu yake anachokipendelea nafsi yake. Angalau kile unachoipendelea nafsi yako umfanyie ndugu yako, na kile nafsi

yako unachokichukia basi kiweke mbali naye. Jihadhari kumpuuza yule mwenye kumuamini Allah kuwa ni Mlezi, Uislamu ndio Dini, na Muhammad Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake ni Mtume na ni Nabii. Hakika hilo amelitahadharisha kwa kusema: *"Yatosha mtu kuwa ni mtu wa shari kwa kumdharau ndugu yake Muislamu."* **[Ameipokea Muslim].**

Ndugu yangu Muislam! Njia ni rahisi na Ibada ni nyepesi nyakati zote. Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema kumuambia Abu Dardaai: *"Hivi nikujuze juu ya Ibada zilizo nyepesi na rahisi zaidi kwa Mwili kiutendaji."* Abu Dardaai akajibu: 'Niambie ewe Mjumbe wa Allah!' Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, akasema, *"Jilazimishe kunyamaza na kuwa na tabia nzuri. Kwani hakika hautafanya chengine mfano wake."*

Malipo ya tabia njema kwa Muumini yanalingana na malipo ya ambaye anasimama usiku mzima na anafunga mchana. Kwa hiyo Muumini kama anavyosema Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, *"Atafikia daraja la mfungaji na mwenye kusimama kuswali usiku - kutokana na Tabia yake njema."* Kwa mazingatio haya alikuwa

Swahaba mtukufu Abu Dardaai akisema: “Hakika mja Muislamu anakuwa na tabia zake njema mpaka tabia zake njema hizo zinamuingiza peponi, na anafanya tabia mbaya mpaka tabia zake mbaya hizo zinamuingiza motoni”.

## Alama za Tabia Nzuri

Hakika zimekusanyika alama za tabia nzuri kwenye sifa nyingi, miongoni mwa hizo ni:

Mwanadamu kuwa na haya nyingi, asiyekuwa na maudhi, mwingi wa wema, msema kweli, mchache wa maneno, mwingi wa matendo, sio mwenye porojo, mwenye kuunga udugu, mwenye subira zaidi, mwenye kushukuru, mwenye kuridhia, mtulivu, mpole, msafi, mwenye kupenda kheri, sio mwenye kulani wala kutusi, wala kufitini na kusengenya, wala hana haraka na mifundo, na wala sio bahili wala hasidi, mwenye bashasha nyingi, anapenda na kuridhia kwa ajili ya Allah na anachukia kwa ajili ya Yake.

Mtu mwenye tabia nzuri anavumilia maudhi, na siku zote huwapa udhuru watu kutokana na makosa wanayoyafanya, na anafanya kila njia ya kujiepusha

kufatilia makosa yao na kutafuta aibu zao. Muumini haiwezekana kuwa na hali yeyote ile katika hali za tabia mbaya.

Nabii kwenye sehemu nyingi katika mafundisho yake anasisitiza umuhimu wa tabia njema, na malipo makubwa ambayo anayapata mwenye kusifiwa kwa tabia nzuri.

Kutoka kwa Usama bin Sharik amesema: "Tulikuwa tumekaa na Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, wakamjia Watu wakasema: "Ni nani anayependeza zaidi kwa Allah - Mtukufu - katika waja wa Allah?" Akasema: *"Ni yule mzuri wao kitabia."* [Ameipokea Twabaraniy].

Kutoka kwa Abdillahi bin Omar - Allah Awaridhie yeye na baba yake, amesema: nimemsikia Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake akisema: *"Je niwaambie aliyekuwa kipenzi wangu zaidi kati yenu, na atakayekuwa karibu yangu zaidi kati yenu kimakazi siku ya kiyama?"* Wakasema, 'Ndio tuambie ewe Mjumbe wa Allah." Akasema: "*Ni yule mzuri wenu kitabia."* [Ameipokea Ahmad].

Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake alisema, *"Hakuna kitu kizito zaidi katika mzani wa*

*mja siku ya kiyama kishindacho tabia nzuri…"* [Ameipokea Ahmad].

## Tabia za Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-:

Hakika alikuwa Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - mfano wa hali ya juu kwenye zile tabia anazowalingania masahaba zake. Mtume alikuwa anapandikiza tabia bora kwa masahaba zake kutokana na mwenendo wake, kabla hajapandikiza tabia hizo kupitia maneno yake ya hikma na mawaidha.

Kutoka kwa Anas Allah amridhie amesema: "Nimemtumikia Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, miaka kumi, ninaapa kwa Allah hajaniambia nyamaza kabisa, wala hajaniambia kwa kitu ambacho nimekifanya kwanini umekifanya hiki na kwanini usinge fanya hivi?" [Ameipokea Muslim]. Na kutoka kwa Anasi Allah Amuwie radhi amesema: "Siku nilikuwa ninatembea pamoja na Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, Mtume akiwa amevaa Joho nzito, akakutana na bedui akamvuta kwa nguvu hadi nikaona shingo ya

Mtume, ikiwa imeathiriwa na upande wa ile nguo, kutokana na kuvutwa kwa nguvu, kisha akasema: *'Ewe Muhammad toa amri nipewe katika mali ya Allah uliyonayo!' Mtume - Rehema na Amani za Allah zimfikie - akamgeukia yule Mwarabu na akacheka na kuidhinisha apewe mali.*" [Ameipokea Bukhary na Muslim].

Aisha Mke wa Nabii Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake aliulizwa mambo aliyokuwa akiyafanya Mtume nyumbani kwake? Mama Aisha akasema, *"Alikuwa akiihudumia familia yake na unapofika muda wa Swala anatawadha na anatoka kwenda kuswali."* [Ameipokea Muslam].

Kutoka kwa Abdillahi bin Haarith amesema: 'Sijawahi kuona yeyote mwenye tabasamu nyingi kama alivyokuwa Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake!" [Ameipokea Tirmidhy].

Tabia bora zenye kujulikana kwa Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake ni kuwa mkarimu wala si bakhili wa kitu chochote kile, ni shujaa ambae harudi nyuma kupigania haki hata siku moja, ni muadilifu hafanyi ubaya kwenye hukumu kabisa, mkweli na muaminifu kwenye Maisha yake yote.

Kutoka kwa Jaabir Allah Amridhie amesema: ‘Hajawahi kuombwa Nabii Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake chochote na akasema: ‘Sitaki’” [Wameafikiana Bukhary na Muslim]. Mtume alikuwa akitaniana na maswaaba zake, kuchanganyika nao, kucheza na watoto wao, kukaa nao karibu sana, kujibu wito, kuwatembelea wagonjwa na anakubali msamaha kwa mwenye kuutaka.

Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake alikuwa akiwaita maswahaba zake kwa majina mazuri wanayoyapenda na wala hakatishi mazungumzo ya yeyote kati yao. Kutoka kwa Qatada amesema: ‘Kipindi ulipokuja ujumbe wa Najashi alisimama Nabii Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake akiwahudumia, maswahaba wake wakamwambia: ‘Sisi tunatosheleza.’ Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, akasema: “*Hakika hawa waliwakirimu jamaa zetu, na ninapenda niwafanyie hivyo.”* Na akasema: *“Hakika mimi ni mja ninayekula, kukaa kama waja wengine, na nikipanda Punda, kuwatembelea maskini na kukaa na mafukara.”*

## Ukweli:

Hakika Muislamu mkweli yupo kwa Mola wake Mlezi, mkweli kwa watu wote, na ni mkweli katika hali zake zote, ni mkweli kwenye maneno yake na ni mkweli kwa vitendo vyake. Allah Mtukufu Anasema: *“**Enyi mlioamini muogopeni Mola wenu na kuweni pamoja na wakweli**”* [Al-taubah: 119].

Kutoka kwa Aisha Allah Amridhie amesema: *“Hakuna tabia iliyochukiza zaidi kwa Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake kama vile kusema uongo…”* [Ameipokea Ahmad].

Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake: aliulizwa, “Hivi Muumini anaweza kuwa Dhalimu (mwenye kudhulumu)?’ Akajibu: ‘*Ndio!*’ Akaulizwa: ‘Muumini anaweza kuwa Bahili?’ Akasema: *‘Ndio!*’ Akaulizwa tena: ‘Je Muumini anaweza kuwa muongo? Akasema: *‘Hapana.*’” [Ameipokea Maliki].

Uongo kwenye Dini ni miongoni mwa machukizo mabaya sana na ndio uongo mkubwa zaidi, na malipo yake ni moto, kwa kauli yake Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake: *“Yeyote mwenye kunizulia uongo (kwenye Dini) kwa kukusudia, basi ajiandalie makazi yake ni motoni.”* [Ameipokea Bukhary].

Dini yetu ya Uislamu inatuhimiza juu ya kupandikiza tabia ya ukweli kwenye nafsi za Watoto ili wakuwe nayo: Kutoka kwa Abu Hurayra Allah Amridhie kutoka kwa Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema: *"Mwenye kumwambia mtoto njoo uchukue hiki, kisha asimpe huo utakuwa ni uongo."* [Ameipokea Ahmad].

Hakika Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake amehimiza umma wake kujiepusha na uongo hata ukiwa ni kwa njia ya utani. Mtume ameahidi kupata nyumba kati kati ya pepo kwa yule ambaye atajiepusha na uongo japo kwa njia ya utani. Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *"Mimi ni mdhamini wa nyumba kati kati ya Pepo kwa yule ambaye ataacha uongo japo ikiwa ni jambo la utani."* [Amaipokea Abuu Daudi].

Mfanyabiashara huenda akasema uongo pale anapotangaza bidhaa yake, Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake ametahadharisha hivyo, kwa kusema: *"Haiwi halali kwa Muislamu kuuza bidhaa huku anajua kosoro ya bidhaa hiyo, isipokuwa inapasa kumueleza mnunuzi kasoro hiyo."* [Ameipokea Bukhary].

# Uaminifu:

Uislamu unawaamrisha wafuasi wake kutekeleza na kutunza Amana mbali mbali, na Mtu amchunge Mola wake kwa kila alifanyalo liwe dogo au kubwa. Muislamu ni muaminifu kwenye kuyatekeleza aliyowajibishwa na Allah, na ni muaminifu katika kuamiliana na watu. Uaminifu ni mtu kujihimu (kupupia) kuifanya kazi aliyokalifishwa kwa ukamilifu mzuri.

Allah Mtukufu Anasema, ***"Hakika ya Allah Anawa-amrisheni mzirudishe (kutimiza) Amana kwa wenyewe, na mnapo hukumu baina ya watu muhukumu kwa uadilifu."*** [Al-nisaa: 58].

Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *"Hawi na Imani (kamilifu) yule ambaye hana uaminifu."* [Ameipokea Ahmad].

Uaminifu haukuwa kama wanavyoufahamu baadhi ya watu kuwa ni kuhifadhi kitu ulichowekewa, isipokuwa Uaminifu una maana pana Zaidi ya hiyo. Kutekeleza Uaminifu ni Mtu kuwa ni mwenye kufanya vizuri kazi yeyote ambayo amekabidhiwa, au wajibu, sawa uwe ni wa kidini au kidunia.

# Unyenyekevu:

Muislamu ni mwenye kunyenyekea pasi na kujidhalilisha. Wala haitakikani kabisa Muislamu kuwa na kiburi. Allah Mtukufu Anasema, *“**Na wafanyie upole wale wanaokufata miongoni mwa Waislamu.**"* [al-Shuaraa: 215].

Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake anasema: *“Hakuwahi yeyote kunyenyekea kwa Ajili ya Allah isipokuwa alipandishwa daraja.”* [Ameipokea Muslim].

Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *“Hakika Allah Ameniteremshia wahyi kuwa kuweni wanyenyekevu mpaka asijifaharishe yeyote yule kwa mwenzake na wala asimdhulumu yeyote yule mwenzake.”* [Ameipokea Muslim].

Miongoni mwa Ishara za kunyenyekea ni: kukaa na mafukara na masikini, kutojikweza mbele yao, kuwa na bashasha na watu, wala asijione kuwa yeye ni mtu bora kuliko mwengine. Hakika alikuwa Mtume Rehena na Amani za Allah ziwe juu yake akifagia nyumba yake na yeye ni Nabii wa Umma huu, akikamua mbuzi, akifua nguo, akila pamoja na mtumishi wake, akinunua bidhaa sokoni na kuwapa

mikono waislamu wadogo na wakubwa, tajiri na masikini.

## Haya:

Hakika kuwa na Haya ni jambo katika mambo ya kiimani. Haya huleta kheri kama alivyosema Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake kupitia mapokezi ya Bukhary na Muslim. Kiigizo cha Muislamu katika hizi tabia njema ni Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake kwa kuwa alikuwa ni mwingi wa Haya. Kutoka kwa Abii Saidi amesema: *"...Pindi Mtume anapoona kitu ambacho anakichukia tunamjua kupitia uso wake."* [Amepokea Bukhary].

Kuwa na Haya kwa Muislamu hakumzuii kuisema haki, au kutafuta elimu, au kuamrisha mema au kukataza mabaya.

Haya haikumzuia Ummu Sulaymu kusema: 'Ewe mjumbe wa Allah, hakika Allah Haoni haya katika Haki, je mwanamke anapoota anawajibika kuoga?' Akasema: *"Ndio pale anapoona maji."* [Ameipokea Bukhary].

Lakini Haya inamzulia Muislam kufanya matendo mabaya, au kuwa na mapungufu kwenye kazi

alizokalifishwa, au kuweka wazi siri za watu na kuwafanyia ubaya.

Kuona Haya mbele ya Allah ni bora zaidi, Muislamu anatakiwa aone Haya mbele ya Muunba wake ambaye Amemleta duniani na Akamneemesha. Aone Haya kuwa na mapungufu kwenye kumtii Allah, au katika kumshukuru kutokana na Neema zake. Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *"Allah ndio Mwenye Haki zaidi kuona Haya (mbele yake) kuliko Watu."* [Ameipokea Bukhary].

# Tabia Mbaya:

## Dhuluma:

Hakika Muislamu wa kweli hamdhulumu yoyote, kwa kuwa Uislamu umeharamisha kudhulumu, Allah Mtukufu Amesema, ***"… na mwenye kudhulumu miongoni mwenu Tutamuonjesha adhabu kubwa.'' [Al-Furqan 19].***

Imekuja katika Hadithi *Al-Qudsi* Maneno Yake Allah Mtukufu: **"Enyi waja wangu nimeiharamishia nafsi yangu kudhulumu, na nikaifanya Dhuluma kuwa ni haramu kwenu nyinyi basi msidhulumu."** [Ameipokea Muslimu].

**Dhuluma zipo aina tatu, nazo ni**:

**1. Mja Kumdhulumu Mola wake**, na inakuwa ni kwa kumkanusha Allah Mtukufu. Allah Aliyetakasika na Mapungufu, Amesema, *''****Na makafiri (waliokanusha) hao ndio wenye kudhulumu.****''* [al-Baqara: 254]. Na inakuwa ni kwa kumshirikisha Allah kwenye Ibada, nako ni kuzielekeza baadhi ya Ibada kwa asiye kuwa Allah. Allah - Mtukufu Amesema, *''****Hakika ushirikina ni Dhuluma kubwa."*** [Luqmaan: 13].

**2. Mja kumdhulumu mja mwenziwe:** Huwa kwa kuwaudhi kwenye heshima zao, au miili yao, au mali zao pasi na haki yeyote. Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *"Muislamu yeyote ni haramu kwa Muislamu mwenzie: Damu yake, mali yake na heshima yake."* [Ameipokea Bukhary].

Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema,*"Yeyote ambaye ana chochote cha dhulma cha ndugu yake Muislamu, ikiwa ni kumvunjia heshima au kitu chochote, basi arudishe leo leo kabla haijafika siku ambayo hakutakuwa na Dinari wala Dirhamu. Itakapokuwa ana jema litachukuliwa kiasi cha alivyomdhulumu, na endapo hana mema aliyoyatenda, hapo yatachukuliwa mabaya ya aliyemdhulumu na kubebeshwa yeye."* [Ameipokea Bukhary].

3. **Mtu kuidhulumu Nafsi yake:** Nako ni kwa kuyatenda yaliyoharamishwa. Allah - Mtukufu Amesema, *"**Na wala hawakutudhulumu lakini walikuwa wamezidhulumu Nafsi zao.**"* [al-Baqarah:57]. Kwa hivyo kuyafanya yaliyoharamishwa

ni kuidhulumu Nafsi, kwani kufanya hivyo kunawajibisha kupata Adhabu kutoka kwa Allah.

## Husda:

Husda ni miongoni mwa tabia mbaya ambazo Muislamu anapaswa kutokuwa nazo kabisa. Kwa sababu ndani ya Husda kuna upingaji wa ugavi wa Allah kwa waja wake. Allah Amesema: ***"Au wanawafanyia Hasadi watu kutokana na yale ambayo Amewapa Allah katika Fadhila Zake."*** [al-Nisaa: 54].

Husda zipo aina mbili:

a) Ni mtu kutamani kuondoka kwa Neema aliyo nayo mwengine kama vile Mali, au Elimu, au Cheo ili azipate yeye.

b) Ni Mtu kutamani Neema za mwenzie ziondoke hata ikiwa yeye hatozipata.

Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *"Tahadharini na Husda, hakika Husda inakula matendo mema kama vile Moto unavyokula (kuteketeza) Kuni au Majani."* [Ameipokea Abuu Daudi].

Wwala si katika Husda kutamani kupata Neema mfano wa alizonazo mwengine pasi na kutamani zimuondokee.

## Kughushi:

Muislamu ni mwenye kuwafanyia wema ndugu zake. Hamfanyii Hadaa yeyote. Bali hupendelea kwa ndugu zake kile akipendacho kwa nafsi yake. Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *"Yeyote mwenye kutufanyia ghishi (Hadaa) basi huyo si miongoni mwetu."* [Muslim].

Katika mapokezi mengine aliyoyapokea Imam Muslim kwamba Hakika Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake alipita kwenye Rundo la chakula, akaingiza mkono wake, akapatwa na unyevunyevu mkononi mwake, akasema: *"Ewe Muuzaji chakula ni nini hii?"* Akasema: "Kimenyeshewa na Mvua ewe Mtume wa Allah." Akasema: *"Kwa nini usiweke juu ya chakula ili watu waone! Yeyote mwenye kufanya Hadaa (kughushi) si katika sisi."*

## Kughurika (kujiona):

Huenda akaghurika Mwanadamu kwa sababu ya elimu yake na ikamfanya ajikweze na kuwadharau wengine, au hata wanazuoni.

Huenda mwanadamu akaghurika kwa mali zake, akajikweza kwa watu kwa sababu hiyo.

Huenda akadanganywa na nguvu zake, au kwa ibada zake na mfano wa hayo.

Lakini Muislamu wa kweli anajiepusha na kujiona na kujitahadhari nao, anakumbuka kwamba hakuna lililomtoa Iblisi peponi isipokuwa ni kujiona kwake. Hilo ni pale Allah Alipomuamrisha kumsujudia Adamu, akasema: '***Mimi ni bora kuliko yeye, kwa kuwa umeniumba kwa moto na umemuumba yeye kwa udongo***." Na ikawa hii ndio sababu ya kutolewa kwenye Rehema za Allah.

Jinsi ya kuitibu tabia hii ni Mtu kujua hakika zile neema alizopewa na Allah leo, ikiwa ni Elimu, au Mali, au Afya njema, na mfano wa hivyo, hakika ya Allah Anaweza Kuviondoa Muda wowote.

# Miongoni mwa Mbinu za Kupata Tabia Njema:

Hakuna shaka kuwa jambo zito kwenye maumbile ya kibinadamu ni kubadilisha tabia ambazo nafsi imeumbwa nazo. Lakini hili si kuwa linashindikana wala haliwezekani. Isipokuwa kuna sababu nyingi, na mbinu mbali mbali, kwa kuzifuata mbinu hizo mwanadamu anaweza kupata tabia nzuri. Miongoni mwa mbinu hizo ni:

## Kusalimika kwa Itikadi:

Itikadi ni jambo kubwa sana, kwani Tabia kwa kawaida yake ni matunda ya kile ambacho anakibeba mwanadamu kifikra, Itikadi anayoitakidi na yale anayoyatekeleza kwenye Dini.

Kisha Itikadi ndio Imani na ukamilifu wa Imani kwa waumini ni yule mzuri wao zaidi kitabia. Endapo Itikadi itakuwa sahihi basi Tabia zinakuwa nzuri kwa kufuata Itikadi. Kwani Itikadi sahihi inampelekea mwenye Itikadi hiyo kuwa na tabia njema, kama vile ukweli, ukarimu, upole, ushujaa na mfano wa hayo. Kama pia Itikadi hiyo inavyomzuia na tabia

mbaya kama vile uongo, kupenda mali, ubahili, ujinga na mfano wa hayo.

## Dua ni Mlango Mkubwa:

Dua ni mlango mkubwa, na pindi unapofunguliwa kwa mja zinafululiza kwake kheri nyingi na kuvuna baraka tele.

Mtu yeyote atayetaka kujipamba na tabia njema na kujiepusha na tabia mbaya, basi ajiegemeze kwa Mola wake ili ampe tabia njema na kumuondolea tabia mbaya. Dua ina faida kwenye hili na mengineyo, na kwa hili alikuwa Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, mnyenyekevu zaidi akimuomba Allah Amruzuku tabia nzuri, na alikuwa akisema kwenye Dua yake ya ufunguzi wa Swala: *"Ewe Allah niongoze kuwa na Tabia nzuri, hakuna muongozaji wa uzuri wake isipokuwa ni wewe, na Uniondolee ubaya wake na hakuna muondoaji wa ubaya wake isipokuwa ni wewe."* [Muslimu].

## Kupambana na nafsi:

Kupambana na nafsi au kujipinda kunafaa sana kwenye suala hili. Hakika yule ambaye atailazimisha nafsi yake kushikamana na mambo mazuri, na akai-lazimisha kujiepusha na mabaya kwa hilo atapata

kheri nyingi, na kumlinda na shari iliyompata. Tabia kuna ambazo hutokana na kimaumbile, na nyengine hupatikana kwa mafunzo na kuzitenda.

Mtu kujipinda haina maana ya mtu kuilazimisha nafsi yake mara moja, au mbili, au zaidi, isipokuwa maana yake ni kuilazimisha nafsi yake mpaka unamkuta umauti. Kwa hili hakika kujipinda ni Ibada na Allah Mtukufu Anasema: *“**Muabudu Mola wako mpaka ukujie umauti.”*** [al-Hijri: 99].

## Kujihisabu na Kujitathmini:

Hii ni kuikosoa Nafsi pale inapofanya tabia mbaya na kuifanya isiweze kurudia kufanya tabia hizo mara nyingine.

## Mazuri ya Tabia Njema:

Hakika kujua matunda mazuri ya vitu na kufikiri kiundani uzuri wa mwisho wake, ni sababu kubwa inayosukuma kufanya matendo mazuri kujifananisha nayo na kujitahidi kuyafanya.

## Kufikiria mwisho wa tabia mbaya:

Nako ni kuzingatia yanayoletwa na Tabia mbaya, miongoni wa majuto yenye kudumu, huzuni

anayodumu nayo, hasara, majuto na kuingiza chuki kwenye mioyo ya wanadamu.

## Kujihadhari na kukata tamaa:

Kukata tamaa si jambo zuri kwa Muislamu na wala siku zote halilingani naye. Muislamu anatakiwa kuyapa nguvu matakwa yake ya kheri, kujitahidi kuikamilisha nafsi yake na kujipinda kuepuka kasoro zake.

## Kujilazimisha kuwa na Bashasha na Tabasamu na kujiepusha kukunja uso:

Hakika mtu kutabasamu mbele ya uso wa ndugu yake Muislamu ni sadaka inayolipwa. Kama Nabii Rehema na Amani ziwe juu yake, alivyosema, *"Kufurahi kwako mbele ya uso wa ndugu yako ni Sadaka."* [Ameikusanya at-Tirmidhy].

Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake, amesema, *"Msipuuzie chochote katika mambo mema, japo kwa kumuonesha ndugu yako Muislamu Uso wenye bashasha."* [Ameipokea Muslim].

## Kusamehe na kujisahaulisha:

Ni miongoni mwa Tabia za wakubwa na watukufu, na sifa hizi mbili ni miongoni mwa sifa zinazobakisha, na kukinga dhidi ya uadui.

## Upole:

Upole ni miongoni mwa tabia tukufu, na inapasa kuwa na tabia hii kwa wenye akili. Nayo ni kuidhibiti Nafsi pale inapopata yenye kuikasirisha. Na wala haina maana kwamba kutokasirika ndio sharti la Upole, isipokuwa mtu pale anapopata yale ambayo ni yenye kukasirisha anajizuia kwa sababu ya upole wake. Mtu anapokuwa na sifa ya upole anapendwa na wengi, wanakuwa wachache wabaya wake na hupandishwa daraja.

## Kupingana na mambo ya kijahilia (yasiyo ya kistaarabu):

Mtu ambaye atapingana na ujahilia atahifadhi heshima yake na kuipumzisha nafsi yake, na atakuwa amesalimika kusikia yanayomuudhi. Allah Mshindi na Mtukufu Amesema, ***"Samehe na amrisha mema na upinge mambo ya wajaahili."*** [al-Aarafu: 199].

## Kujiepusha na kugombana na watu.

### Kusahau maudhi:

Nako ni kusahau maudhi mabaya yaliyokupata ili uusafishe moyo wako na wala usiudhike. Na yule mwenye kukumbuka mabaya ya ndugu zake hatokuwa na mapenzi nao. Mtu atakayekumbuka maovu aliyofanyiwa na watu hatoishi nao Maisha mazuri. Hivyo, sahau yao uwezavyo kuyasahau.

### Kusamehe na kubadili baya kwa jema:

Na hii ni sababu ya kuwa na nafasi ya juu, utulivu na kuiondoa Nafsi katika kulipa kisasi.

### Ukarimu katika kutoa:

Ukarimu ni sifa nzuri inayoheshimiwa na jamii. Na ulivyo ubahili ni sifa mbaya yenye kuchukiwa. Utoaji unaingiza upendo na kuondoa uadui, unaleta ukumbusho mzuri na unaficha kasoro na maovu.

### Kutegemea malipo kwa Allah:

Jambo hili ni kubwa miongoni mwa yanayosaidia kupata tabia bora, kwa kuwa ni miongoni mwa yanayosaidia kuwa mvumilivu, kujipinda, na kuvumilia maudhi ya watu. Pindi mwanadamu anapokuwa na yakini kwamba Allah Mtukufu

atamlipa kwa tabia zake nzuri, na kuilazimisha nafsi yake (kuwa mwema), hakika atafanya pupa kuwa na Tabia nzuri na yatakuwa mepesi yale anayokutana nayo katika kutekeleza hilo.

## Kujiepusha na Hasira:

Kwa hakika Hasira ni kaa la moto linalowaka kwenye moyo, linapelekea kupenda ukubwa na kutesa watu. Na kuiepuka hasira, ni mtu kuidhibiti Nafsi yake wakati wa Hasira zinapomjia. Hakika mtu anayefanikiwa katika hili atakuwa ni mwenye kuhifadhi ushindi na utukufu wa Nafsi yake, na atakuwa anaiepusha na udhalili wa kuomba radhi kwa makosa na ubaya wa majuto. Kutoka kwa Abi Hurayrah Allah Amridhie amesema: "Alikuja Mtu akasema: 'Ewe Mtume wa Allah, Niusie.' Akamuusia: '*Usikasirike.*' Kisha akarudia mara nyingi kuomba usia, Akamuusia tena: '*Usikasirike.*'" [Ameipokea Bukhary].

## Kukubali nasaha zenye lengo zuri, na kukosoa kwa kujenga:

Muislamu pale anapogundua yale ambayo yana mapungufu katika nafsi yake inampasa kuifanya

Nafsi yake ni yenye kuyaepuka, kwani kuitengeneza Nafsi hakutimii bila ya kujua kasoro zake.

## Mtu kusimamia majukumu aliyopewa kikamilifu na kwa usahihi.

Hili litamuepusha na kukaripiwa na kukemewa, Muislamu anatakiwa ajisalimishe na udhalili wa kuomba radhi.

## Kukubali kosa linapotokea, na kuchukua tahadhari dhidi ya kulihalalisha:

Kufanya hivyo ni alama ya Tabia njema, kisha kunakusalimisha na uongo. Kukubali kosa ni jambo zuri, linampandisha Mtu cheo.

## Kulazimiana na ukweli:

Hakika ukweli una athari nzuri, na kupitia ukweli kinapanda cheo cha mtu, na nafasi yake katika jamii huwa juu. Ukweli unamuokoa Mtu na uchafu wa uongo na dhamira mbaya na udhalili wa kuomba radhi. Ukweli unamlinda dhidi ya kufanyiwa ubaya na watu na kuondoka uaminifu wake. Ukweli pia unampa utukufu, ushujaa na kujiamini.

## Kujiepusha na kulaumu sana na kumkaripia yule ambaye amekosea:

Kulaumu sana kunatia hasira, kunaleta uadui, na pia ni sababu ya kusikia yanayoudhi. Kwa mwenye akili nzuri hawezi kuwaadhibu ndugu zake kwa dogo na kubwa, isipokuwa anawachukulia na kuwapa Udhuru. Kama endapo kutakuwa na yanayo lazimika kukemea basi iwe kwa ulaini na upole.

## Kufuatana na Watu wema na wenye Tabia njema:

Jambo hili ni miongoni mwa mambo makubwa yanayokuza na kuithibitisha tabia njema kwenye Nafsi ya mtu.

## Kuchunga Adabu za mazungumzo na vikao:

Miongoni mwa Adabu zake ambazo zinapaswa kuzichunga vizuri ni kumsikiliza anayekuzungumzisha, na kujiepusha kukatisha mazungumzo yake, au kumuona muongo, au kumdharau, au kuondoka kabla ya kukamilisha mazungumzo yake.

Miongoni mwazo pia, ni kusalimia pale unapoingia na unapotoka, na kupeana nafasi kwenye vikao, na

wala mtu asimsimamishe mwengine na kukaa yeye sehemu yake. Wala asiwatenganishe waliokaa pamoja isipokuwa kwa idhni yao. Pia wasiongee kwa siri wawili bila ya kumshirikisha mwenzao wa tatu.

## Kudumisha kusoma mwenendo wa Mtume Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake:

Mwenendo wa Mtume unamuwekea msomaji wake mtazamo mkubwa ulioutambua ubinadamu, uongofu na Tabia kamilifu kwenye Maisha ya kibinadamu.

## Kuangalia ki undani mienendo ya Maswahaba watukufu Allah Awaridhi.

Kujua na kuyasoma maisha ya masahaba na kuiga mienendo yao ni sababu kubwa ya kuongoka na kuishi maisha ya furaha na amani. Pia ndio njia pekee ya kuishi kulingana na Mafundisho ya Qur’an na Sunna na hivyo kutupelekea sisi kupata Radhi za Allah.

## Kusoma vitabu vya Tabia:

Vitabu vya tabia njema humzindua mwanadamu juu ya tabia mbalimbali zilizo njema. Vitabu hivyo pia

vinamkumbusha ubora wake na kumsaidia kuzipata tabia njema. Pia vinamkumbusha tabia mbaya, kumbainishia mwisho mbaya na njia za kuziepuka Tabia mbaya hizo.

## Fihrisi ya Kitabu

Utangulizi ....................................................................3
Alama za Tabia Nzuri ...........................................................8
Tabia za Mtume (s.a.w) .......................................................10
Ukweli...............................................................................13
Uaminifu ............................................................................15
Unyeyekevu .......................................................................16
Haya ..................................................................................17
Tabia Mbaya ni: .................................................................19
Dhuluma: ...........................................................................19
Husda: ...............................................................................21
Kughushi (Kufanya Hadaa): ...............................................22
Kughurika (Kujiona):..........................................................23
Miongoni mwa Mbinu za Kupata Tabia Njema .....24
Kusalimika Itikadi ..............................................................24
Dua: ..................................................................................25
Kupambana na Nafsi ..........................................................25
Kujihisabu na Kujitathmini ................................................26
Kuzingatia Matokeo Mazuri ya Tabia Njema .....26
Kufikiria Mwisho Mbaya wa Tabia Mbaya ........26
Kujihadhari na Kukata Tamaa ............................27
Kujilazimisha Kuwa na Bashasha .......................27
Kusamehe na Kujisahaulisha ..............................28
Upole .................................................................................28
Kupingana na Mambo ya Kijaahilia ...................28

Kujiepusha na Kugombana na Watu. ..................29
Kusahau Maudhi.................................................29
Kusamehe na Kufuta Kubadili Baya kwa Jema.. 29
Ukarimu katika Kutoa .......................................29
Kutegemea Malipo Kwa Allah ...........................29
Kujiepeusha na Hasira.......................................30
Kukubali Nasaha zenye Lengo Zuri ....................30
Mtu Kusimamia Majukumu Kikamilifu………. 31
Kukubali Kosa Linapotokea ...............................31
Kulazimika na Ukweli........................................31
Kujiepusha na Kulaumu Sana ............................32
Kufuatana na Wema na Wenye Tabia Njema .....32
Kuchunga Adabu za Mazungumzo na Vikao......32
Kudumisha Kusoma Mwenendo wa Mtume .......33
Kuangalia Ki Undani Mienendo ya Maswaaba...33
Kusoma Vitabu vya Tabia.................................33